JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - TAMISEMI

Namba za simu
Mkuu wa shule: **0757995160**
Makamu mkuu wa shule: **0767071402 AU 0712600755**
Matron/Patron: ________________

Shule ya Sekondari Mawelewele,
S.L.P 459,
IRINGA.

Kumb. Na. IR/MAWSS/FV JIN/2023

Tarehe 12/06/2023.

USAJILI NECTA: S1161

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi,

............................................

S.L.P....................................

……………………………….

**YAH : MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MAWELEWELE MANISPAA YA IRINGA MKOA WA IRINGA MWAKA-2023/2024 (BWENI)**

**1. UTANGULIZI:**

Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka **2023/2024** tahasusi ya ………... Nafasi hii ameipata kwa sadaka ya wananchi na Taifa, si kwa uwezo wake tu. Aitumie kwa bidii, uaminifu na shukrani kubwa. Aidha anapaswa ajue na kukumbuka kila mara kuwa yeye sasa anaandaliwa kwa namna ya pekee kulitumikia Taifa, jamii na yeye mwenyewe kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Shule hii ipo umbali wa km.4.6 upande wa magharibi kutoka Iringa mjini kuelekea ofisi za mkuu wa wilaya mtaa wa Kigamboni na inapakana na kituo cha watoto yatima cha Huruma Centre na chuo cha Biblia cha Amani (Anglican). Usafiri wa Bajaj kutoka mjini unapatikana kwa nauli ya Tsh. 500/=

Moto wa shule yetu ni "AMANI NA MAENDELEO" na kauli mbiu yetu ni "PIGA VITA UJINGA, KUBWETEKA, MAFARAKANO NA MASHAKA". Tukiwa na kauli hizi mbili kama kiini cha dira yetu tunategemea utakuwa mwanafunzi mwelekevu, hodari, mchangamfu na mzalendo daima uwapo mmoja wa wanamawelewele popote pale. Mawelewele ni shule yako, kaka yako, dada yako, baba yako, tena ni mama yako, msikilize, mheshimu naye atakuletea mafanikio ukachanue.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 14/**08/2023**, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 13/08/2023 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023 baada ya hapo mwanafunzi hatapokelewa.
**Shule yetu ina tahasusi (Combinations) zifuatazo**:
PCB, CBG, HGL, EGM na HKL. Kadhalika tunafundisha General studies, Basic Applied Mathematics (BAM) na Dini kadiri ya dhehebu la mtoto na vipindi vya ushauri nasaha ambavyo hufanyika pia nje ya saa za masomo.

Shule yetu ni ya mchanganyiko, wasichana na wavulana kuanzia kidato cha kwanza hadi nne na ni ya kutwa, na ni bweni kwa kidato cha tano na sita wavulana tu. Wazazi na wanafunzi ni tegemeo kubwa katika kuboresha mazingira ya kujifunza kwa sababu hiyo ushiriki wao kwa hali na mali unahitajika mara kwa mara.

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**Unapokuja shuleni tafadhali zingatia na chukua tahadhari zote dhidi ya ugonjwa wa COVID -19 unaosababishwa na virusi vya CORONA.**

## Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB: Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na BIMA YA AFYA kama hana aje na tsh. 50,400/= kwa ajili ya bima**

**NB:- MALIPO YOTE YAFANYWE KUPITIA A/C No. 60501100035 NMB, jina la A/C ni "MAWELEWELE SECONDARY SCHOOL" (isipokuwa fedha ya bima).** Michango hii inatakiwa kulipwa yote bila kupungua mwanafunzi anaporipoti shuleni muhula wa kwanza kabisa. Mwanafunzi anaporipoti ni lazima aje na Bank Pay Slip (BPS) original iliyoandikwa; **jina la mwanafunzi na kidato** na Siyo jina la Mzazi au mlezi aliyelipia**.**

A. VIFAA VYA KULETA SHULENI

Mwanafunzi anatakiwa kuleta vifaa vifuatavyo:

1) **Vifaa vya usafi**, kila mwanafunzi anatakiwa aje na fagio laini (soft broom), squizer moja pamoja na
   - Reki yenye mpini wa chuma kwa wanafunzi wa PCB na CBG
   - Mkasi wa kukatia maua kwa wanafunzi wa HKL
   - Jembe moja lenye mpini lililonolewa kwa wanafunzi wa HGL na EGM

2) **Vifaa kwa ajili ya matumizi binafsi** ambapo kila mwanafunzi anapaswa kuja na :-
   - Godoro moja futi $2\frac{1}{2}$ x 6
   - Sahani, bakuli, kijiko, mswaki na kikombe
   - Ndoo moja (1) ya plastic ya lita 10
   - Blanketi moja, shuka mbili rangi ya blue bahari, mto na foronya rangi ya blue pamoja na taulo
   - Chandarua
3) **Mahitaji muhimu ya darasani**:
   - Daftari Counter books zisizopungua saba (7).
   - Vitabu vya masomo ya tahasusi husika angalia orodha iliyoambatanishwa.
4) Rimu mbili (2) za karatasi nyeupe A4 (kila rimu iwe na karatasi 500) kwa kila mhula (rimu nne (4) kwa mwaka)
5) Picha tatu (3) za passport size za rangi (zilizopigwa ndani ya miezi sita)
6) Nakala (copy) za vyeti vifuatavyo.
   - Cheti cha kuzaliwa
   - Form Four Leaving Certificate (Cheti cha kuhitimu kidato cha nne)
   - Results slip ya kidato cha nne (Original na nakala yake).
7) Spring/Flat File moja (1) - **Hatupokei box file**.
8) Mahitaji muhimu ya tahasusi (combinations)
   - Dissecting kit, white laboratory coat na stop watch kwa wanafunzi wa tahasusi za PCB na CBG.
   - Electronic Scientific Calculator fx-991 na Complete Mathematical set kwa wanafunzi wa tahasusi za PCB, EGM na CBG.
   - Advanced Learners' Dictionary - Oxford kwa wanafunzi wa tahasusi za HGL na HKL

3. **SARE ZA SHULE**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na sare kama ifuatavyo:

A. Mashati **mawili** meupe ya tetron ya mikono mirefu. Yawe ya mshono wa kawaida na mfuko mmoja.
B. Suruali **NNE (4)** za malinda mawili kila moja (isiwe modal kufuata umbo la mtu). Mbili za rangi ya **ugolo [brown]** zitatumika kama uniform wakati wa masomo na mbili za rangi **khaki** (ambazo ni shamba dress)
C. Tai iwe ni ya rangi ya **ugolo** (**brown**).
D. Viatu vyeusi vya ngozi **jozi mbili** vyenye visigino vifupi vya **kufunga na gidamu** (kamba) visivyo chongoka mbele na soksi **nyeusi**
E. Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi usio na marembo yoyote zaidi ya weusi.
F. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na mavazi ya michezo:- raba nyeupe, Track suit ya rangi ya bluu bahari, Jezi ya dark blue.
G. Sweta rangi ya bluu lenye shingo ya V na Koti jeusi lisilo na maandishi kwa nyakati za baridi baada ya muda wa masomo.
H. T-shirt ya kijivu aina ya "Form six" ( Unaweza kuipata Jirani na shuleni kwa gharama ya Tsh. 15,000/=)
I. Vifaa vyote hivi vitakaguliwa siku ya usajiri.

4. **VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU:**

Unapaswa kuja na fomu zilizoambatanishwa na barua hii zikiwa zimejazwa kikamilifu ambazo ni:-

**A.** Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical examination Form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.
**B.** Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na kukiri kwa mzazi/mlezi kukubaliana na sheria, kanuni, michango mingine na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
**C.** Fomu ya kukubali mabadiliko ya adhabu

5. **USAFI BINAFSI:**

Mwanafunzi awapo popote anategemewa kuwa msafi, kimwili, kimawazo na kimatendo. Achane nywele zilizonyolewa kwa mtindo wa kawaida sio kwa mitindo ya mitaani. Atumie lugha kiungwana na daima ahakikishe kuwa hawi kero kwa wenzake. Mwanafunzi haruhusiwi kupaka rangi kucha, kuacha kucha ndefu , kusuka nywele na urembo wa aina yoyote kwa muda wote awapo shuleni.

6. **ANGALIZO NA MSISITIZO:**

Shuleni ni mahali pa kujifunza. Ni mahali pa kujipatia stadi njema, kujijengea utu wema na kujisomea. Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vipindi vyote na kutekeleza maagizo na maelekezo ya walimu na walezi wake kikamilifu na kwa wakati. Aidha azingatie kuwa **lugha rasmi ya mawasiliano shuleni ni kiingereza**!. Ratiba ya shule huanza saa 1.00 asubuhi na kuishia saa 9.30 kila siku isipokuwa siku ya Ijumaa huishia saa 6.30 mchana kutoa nafasi kwa swala ya Ijumaa kwa Waislamu. Wengineo wanaweza kuendelea hadi saa 9.30 kwa maelekezo ya walezi wao wa Dini. Aidha jioni kwa siku muafaka kutakuwa na michezo na shughuli mbalimbali za elimu kwa vitendo kwa madarasa na vikundi mbalimbali hadi saa 11.00 jioni kadri itakavyopangwa na walimu husika.

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

➢ **Mkuu wa shule 0757995160 Makamu Mkuu wa Shule 0767071402/0712600755.**
➢ **Mwandamizi Taaluma 0752333115 Mwandamizi Malezi 0764620214**

**R. M. NGIMBA**
**MKUU WA SHULE**

HEADMASTER P.O. BOX 459 IRINGA DATE MAWELEWELE SEC. SCHOOL

OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA IRINGA

# SHULE YA SEKONDARI MAWELEWELE

S. L. P. 459, IRINGA - TANZANIA

IR/MAWS/64/2

Mwanafunzi mpendwa,
Shule ya Sekondari Mawelewele,
S.L.P. 459,
**IRINGA.**

**SHERIA ZA SHULE**

Binadamu wakaapo pamoja huwa wana lengo maalum. Taasisi ya elimu kama yetu ina malengo mahsusi ili kuyafikia malengo hayo hakuna budi kuwa na utaratibu wa kuufuata. Kwa minajili hiyo mwanafunzi yeyote wa shule hii anapaswa kutekeleza yafuatayo sambamba na desturi nyingine za waungwana wa kitanzania.

A. **MAHUDHURIO NA KUTHAMINI MUDA**:

Kila mwanafunzi anapaswa kuthamini muda na kuwapo mahali anapotakiwa kwa wakati kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

1. Kuwahi kufika shuleni na kuwa mstarini saa 1:20 kila siku ya masomo.
2. Kuhudhuria vipindi vyote vya siku. Sababu za kuondoka katika kipindi hazihalalishi kukosa kwako somo na zinaiba wakati wako.
3. Kuhudhuria mikutano, semina, warsha na makongamano yote yale yanayoandaliwa na kuidhinishwa na uongozi wa shule.
4. Kutambua na kuitika mara moja miito mbalimbali halali ikiwa ni pamoja na ile ya dharura. Ni mwiko kumpa kisogo mwalimu pale unapoitwa au kutakiwa kufanya jambo lolote. ***Amkimbiaye mwalimu hukimbia elimu na busara akheri asingalijiunga nasi.***

**B. HESHIMA NA ADABU**

Mwanafunzi anapaswa kudhihirisha adabu na heshima kwa wote na popote pale anapokuwapo na hivi yampasa:

1. Kuwathamini na kuwaheshimu wanafunzi wenzake wote na wale wote wanaomzidi umri. Aonyeshe unyenyekevu mbele ya wakubwa na kuwastahi watu wote na hasa wale anaodhani na kuona amewazidi kwa namna moja au nyingine.
2. Kusimama na kumsalimu mwalimu na mtu yeyote hasa anayemzidi umri anapopita, unapompita au unapoingia mahali alipo.
3. Kutumia lugha nzuri wakati wote.
4. Kuthamini na kuheshimu kazi zote kisha kuonyesha ushirikiano na wenzio kazini.
5. Kuheshimu mali yake na ya mwezie na hasa ya umma. **Kumbuka hakuna kitu kisichokuwa na mwenyewe.**
6. Kunyosha mkono unapoomba, kuuliza au kujibu swali.
7. Kukaa kimya darasani na kutoka mahali ulipo kwa ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyepo. Mizaha mingi na vichekesho visivyohusiana na somo hupoteza muda na kuvuruga fikara.
8. Kuacha kabisa tabia za kihuni na potofu kwa rijali ikiwa ni pamoja na
   - Kuvuta sigara, kutumia vileo kama pombe na dawa za kulevya.
   - Kufuga kucha ndefu, kufuga ndevu na nywele ndefu

- Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima na yanayobana mwilini.
- Kuvaa nguo chafu zilizochanika na zinazokera wenzio pia kutooga, kutopiga mswaki na hivyo kutoa harufu mbaya
- Kugombana, kusema kwa jazba na kudharau hata kwa kukonyeza tu.
- Kuendekeza vitendo vya ngono na viashiria vyake kama kupapasana, kukonyezana na kuandikiana barua za mapenzi. Kujiingiza katika vitendo vihusianavyo na hayo huhamisha mara moja juhudi zako katika masomo na kusababisha anguko la ghafla kitaaluma.
- Wizi, utapeli, kamari .

**C. MATUMIZI YA SARE NA KITAMBULISHO CHA SHULE**

Kila mwanafunzi kama ilivyo kwa kila mtu anapaswa kuwa na kitambulisho na kutembea nacho popote aendapo. Hiyo ni tabia njema ambayo kila muungwana anapaswa kupalilia na kuijenga. Kutokuwa na kitambulisho rasmi kunasababisha usumbufu mwingi. Mwanafunzi una haki zako za msingi za kiupendeleo katika jamii jitambulishe mara moja utendewe ipasavyo. **Kitambulisho kitatumika wakati wote wa mitihani.**

Unapaswa kuwa na sare ya shule kwa mshono uliokubalika na kuivaa kila wakati unapopaswa kama vile wakati wa masomo, safarini kwa jina la shule, wakati wa kwenda popote kwa ruhusa ya shule na kunako maandamano yaliyoruhusiwa na uongozi wa shule. Wakati wa michezo washangiliaji wavae vazi rasmi na wachezaji wawe katika sare za michezo.

**D. MIPAKA YA SHULE NA MAENEO MARUFUKU:**

Kila mwanafunzi anapaswa kufahamu fika mipaka ya shule na kutoivuka awapo shuleni. Kadhalika atambue vema maeneo marufuku kwake na ajali kutoyatembelea kwa manufaa yake. Pasi maalum itatolewa na Makamu wa Mkuu wa Shule au Mwalimu wa Malezi ikibidi wewe uivuke au uingie katika maeneo hayo. **Kila ruhusa itaripotiwa kwa Mwalimu wa zamu kwa idhini ya mwisho ya kuondoka shuleni.**

Kwa kutekeleza hayo wanafunzi wasiende bila kibali sehemu zifuatazo
- Ofisi na nyumba za walimu na wafanyakazi
- Maabara, Bohari na Maktaba

Aidha hairuhusiwi kwa mwanafunzi kutembelea maeneo marufuku ikiwa ni pamoja na:
- Vilabu vya pombe na baa
- Nyumba za starehe na kumbi za muziki/dansi
- Nyumba za kufikia wageni bila kuandamana na mlezi/mzazi halali

E. **MAKOSA YANAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**:

Yafuatayo ni baadhi ya makosa yanayoweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ikiwa ni pamoja na makosa yote ya jinai
- Wizi au uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
- Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa (Utoro sugu)
- Kugoma ama kuhamasisha mgomo.
- Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
- Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
- Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni. (Hairuhusiwi kusuka nywele au kuweka dawa kwenye nywele)
- Kufuga ndevu.
- Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya au kuuza dawa za kulevya.
- Uvutaji wa sigara.
- Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
- Kupata au kusababisha mimba na au kutoa mimba.

- Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
- Kutembelea nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
- Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
- Kudharau bendera na alama za Taifa
- Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
- Makosa madogo madogo yanayorudiwa rudiwa kila mara

**F. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA MWANAFUNZI AWAPO SHULENI:**

1. Mwanafunzi hataruhusiwa kuwa nje ya shule ila kwa ruhusa maalum ya mkuu wa shule, na atatakiwa kurudi shuleni ifikapo au kabla ya saa 12:00 jioni.
2. Shule hii ni ya serikali kila mwanafunzi atambue kuwa akiwa shuleni hatakuwa tofauti na wanafunzi wengine kwa misingi ya kidini, kikabila na kiuchumi.hivyo hakuna chakula maalum kwa mwanafunzi, wanafunzi wote watakula chakula kinachoandaliwa shuleni
3. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kujadili dini au siasa ya mwingine, wala hairuhusiwi kuwa na mjadala wa kidini au kisiasa hapa shuleni, kwani shule haina kanisa wala msikiti, ukikwaji wa maelekezo haya yatasababisha mwanafunzi kuondolewa shuleni mara moja.
4. Katika siku za ibada (Ijumaa, Jumamosi na Jumapili) wanafunzi wataruhusiwa kwenda katika nyumba za ibada zilizojirani na shule na zitakazoainishwa na walezi wao.
5. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kutoka darasani na kwenda ibadani muda wa vipindi vya darasani. Aidha ratiba ya masomo hairuhusu mwanafunzi kutoka kwenda kambi au kongamano za kidini wala kufanya shughuli za kidini wakati shule inaendelea. Walimu wa dini na madhehebu yote wanapaswa kutoa mafundisho yao muda wa vipndi vya dini na siku za ibada, pasiwepo na mwingiliano wa aina yoyote na ratiba ya shule
6. Wanafunzi wote wanapaswa kuvaa sare ya shule wanapotoka nje ya shule. Nguo yoyote hairuhusiwi.
7. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuchelewa tarehe ya kufungua shule, akichelewa atapaswa kutekeleza adhabu kama zinavyoonyeshwa katika fomu ya mabadiliko ya adhabu.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

NB: MWANAFUNZI AJENGE UTARATIBU WA KUSOMA MARA KWA MARA MAELEKEZO YALIYOPO KWENYE FOMU HII.

**Tunakukaribisha sana na kukutakia daima amani na maendeleo!**

OFISI YA YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA IRINGA

# SHULE YA SEKONDARI MAWELEWELE

S. L. P 459, IRINGA - TANZANIA

## FOMU YA KUANDIKISHWA

**(a) Ijazwe na mwanafunzi: (Bandika picha sehemu uliyotengewa)**

PICHA YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la mwanafunzi ______________________________
2. Uraia ______________________________
3. Dini ____________ Dhehebu ______________
4. Tarehe ya kuzaliwa ______________________________
5. Mkoa aliozaliwa ______________________________
6. Yatima / Sio yatima ______________________________
7. Kata unayoishi ______________________________
8. Shule za msingi na sekondari alizosoma kabla ya kuja Sekondari ya Mawelewele

| JINA LILILOANDIKISHWA SHULENI | SHULE YA MSINGI/ SEKONDARI | TAREHE NA MWAKA ALIOANZIA | TAREHE NA MWAKA ALIOTOKA |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | | | |
| 3. | | | |
| 4. | | | |

**(b) Maelezo binafsi ya Mzazi / Mlezi (Ibandikwe picha ya mzazi/mlezi sehemu uliyotengewa)**

PICHA YA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la Mzazi / Mlezi ______________________________
2. Uraia ______________________________
3. Sehemu unayoishi ______________________________
4. Mtaa ______________________________
5. Namba ya nyumba ______________________________
6. Namba ya simu ______________________________(ya haraka)
7. Jina la ndugu wa karibu wa mwanafunzi hapa mjini Iringa.
   - i) Jina ______________ Simu__________Uhusiano ____________
   - ii) Jina ______________ Simu__________ Uhusiano ____________
8. Jina la Mwajiri wa mzazi/mlezi na Idara ______________________________
   - Anuani : ______________________________
   - Namba ya simu : ______________________________
9. Kazi ya mzazi / mlezi : ______________________________ Mfano : Karani, Meneja, Mwalimu n.k.

**Sahihi ya mzazi / mlezi ______________________________**

**(c) Tamko la Mzazi/Mlezi**

Mimi…………………………………………… ninakubaliana na maelekezo yaliyotolewa na ninakubali mwanangu asome katika shule hii na naahidi kumtimizia mwanangu mahitaji yote yanayotakiwa ikiwa ni pamoja na kulipa michango kwa wakati na kushirikiana na Uongozi wa shule katika kuboresha masomo na mwenendo wa mwanafunzi huyu.

Saini ya Mzazi/Mlezi ………………………………

## SHULE YA SEKONDARI MAWELEWELE
## TAARIFA YA MABADILIKO YA ADHABU KWA WANAFUNZI KUANZIA JANUARI 2020

### UTANGULIZI

Sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978, sheria ya Elimu namba 5 ya mwaka 2007na kanuni ya nne ya Elimu ya 2014 zimeainisha bayana makosa yanayoweza kusababisha mwanafunzi kusimamishwa au kufukuzwa shule.

Bodi ya shule kama chombo kilichoundwa kisheria bado kinaendelea kutekeleza matakwa ya sheria hizi, kwa kuzingatia sheria ya Elimu namba 5 ya 2007 inayotoa mamlaka kwa bodi ya shule kufanya mabadiliko ya sheria, kanuni na taratibu za shule. Bodi katika kikao chake cha tarehe 03/10/2019 ilifanya mabadiliko kwa baadhi ya adhabu kwa wanafunzi watovu wa nidhamu baada ya kuona kuwa adhabu zinazotolewa hazileti mabadiliko chanya kwa wanafunzi. Mfano wanafunzi wanaopewa adhabu ya kusimamishwa masomo kwa muda huwa wanafurahia kwenda kukaa nyumbani na baada ya kumaliza kutumikia adhabu hiyo warudipo shule hawaonyeshi mabadiliko yoyote.

Pamoja na hayo bodi ilibaini kuwa walimu wanatumia muda mwingi kuwajadili wanafunzi watovu wa nidhamu. Pia wanafunzi wanapopewa adhabu, baadhi ya wazazi/walezi wanaonekana kutokuwa makini katika kusimamia na kufuatilia nidhamu ya watoto wao. Mabadiliko hayo ni kama ifuatavyo:-

A. Mwanafunzi atakayejihusisha na mapenzi ikithibitika adhabu yake ni tofali ndogo za kuchoma 3,000 ndani ya siku 14

B. Kuchelewa kuripoti shule kutoka likizo, adhabu yake ni kuleta ream moja ya karatasi 500 kwa kila siku aliyochelewa (kwa uchelewaji wa siku 5 au pungufu). Zaidi ya siku 5 ataleta tofali ndogo za kuchoma 3000

C. Kuchelewa kuripoti shule baada ya kuruhusiwa kutoka nje ya mipaka ya shule (baada ya saa 12 jioni), ikithibitika adhabu yake ni fagio moja kubwa ya chelewa.

na kuchelewa baada ya vipindi kuanza saa1:40 asubuhi adhabu yake ni fagio moja laini ya sh. Sh. 3,000/=

D. Kugoma adhabu, ikithibitika adhabu yake ni saruji yenye thamani ya tofali ndogo za kuchoma 3,000

E. Kutovaa sare ya shule, ikithibitika adhabu yake ni kuleta saruji mfuko mmoja

F. Kukutwa na simu au kifaa cha simu maeneo ya shule, ikithibika adhabu yake ni tofali ndogo za kuchoma 3,000

NB: ***Adhabu zote hizi zitapaswa kutekelezwa ndani ya siku 14 kwani zaidi ya hapo adhabu itaongezeka***

**AHADI YA KUKUBALI MABADILIKO YA ADHABU**

Nimesoma, nimeelewa na ninakubaliana na mabadiliko ya adhabu yaliyotolewa na Bodi ya shule. Ninaahidi kwamba **nipo tayari kutumikia adhabu hizo/nipo tayari kwa mwanangu kutumikia adhabu hizo**, mara itakapobainika kufanya makosa yaliyotajwa hapo juu

(i) Jina la mwanafunzi__________________ kidato……….. sahihi………….. Tarehe ……..

(ii) Jina la Mzazi/mlezi …………………………….. Namba ya simu………………….. Sahihi ……….

Mahali anapoishi: Mtaa/Kijiji …………………. Kata………………. Wilaya…………………

**SHAHIDI WA AHADI**

(i) Jina la Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji ………………………….

Na. ya simu ……………… Sahihi……………. Tarehe…………….. Mhuri ……………..

(ii) Jina la Afisa Mtendaji wa Kata ………………………….

Na. ya simu ……………… Sahihi…………………… Tarehe…………….. Mhuri ……………..

TANBIHI: **Fomu hii lazima irudishwe shuleni ikiwa imesainiwa na wahusika wote**

R.M. NGIMBA
**MKUU WA SHULE**

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
IRINGA MUNICIPAL COUNCIL

# MAWELEWELE SECONDARY SCHOOL

BOX 459, IRINGA

To be completed by a Government Medical Officer and returned to the Headmaster of Mawelewele Secondary School, P. O. Box 459, IRINGA.

To the Medical Officer, Date: ___________________

_________________________________
_________________________________
_________________________________

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF ……………………………………………….**

Please examine the above named youth as to his fitness to pursue Advanced Secondary School classes as well as conduct other extra curricula activities as a student.

**R. M. NGIMBA**
**HEADMASTER**

**MEDICAL OFFICER'S RECOMMENDATION:**

I __________________________have examined the above named student and considered that he/she is physically fit/unfit to pursue full time secondary studies.

(a) Eye sight __________________________________________
(b) Limbs _____________________________________________
(c) Hearing ___________________________________________
(d) Pregnancy (For Girls) ________________________________
(e) Speech ____________________________________________
(f) Venereal disease _____________________________________
(g) Leprosy ____________________________________________
(h) Epilepsy ___________________________________________
(i) Other problems _____________________________________________________________

___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________

Date _______________________________ Signature __________________________

Station ______________________________ Designation _________________________

**OROdha YA VITABU MUHIMU KWA KILA SOMO**

Unashauriwa kumnunulia mwanao vitabu kulingana na masomo anayosoma .Orodha ya vitabu vinavyotakiwa kwa kila idara ni kama ifuatavyo;

GENERAL STUDIES

1. General studies for Advanced Level Certificate, Form Six (6) by Richard R.F.Mbalase (2011)
2. General studies for Advanced Level Certificate, Form Five (5) by Richard R.F.Mbalase (2011)
3. Contemporary Approach for Advanced Level " General Studies Notes"Form 5&6 by Nyambari C.M Nyangwine, Godfrey Rutta Nyangwine, Steven O. Maluka (New syllabus(2009)

HISTORY

1. Major Issues in African History by Tanzania Institute of Education
2. History of Modern Europe by Peacock
3. How Europe Underdeveloped Africa by W. Rodney
4. History in Focus; Modern World History by Ben Walsh
5. Matering Advanced Level History Book Two, by Kato, A(2011)
6. Matering Advanced Level History Book One, by Kato,A(2012)

GEOGRAPHY

1. Principles of Physical Geography by Monkhouse (2008)
2. Landforms in Africa by Collin Buckle
3. Statistics Simplified by N.A.Saleem
4. Map Reading by Mac Master
5. Human and Economic Geography by C.Morgan (1982)
6. Map reading, General Publications Ltd - Dsm by Durra, S.E. (2003)
7. Geography An Intergrated Apprpoach; Fourth edition by David Waugh (2009)
8. Practical Geography for AFRICA by John .M.Pritchard (1990)
9. R.B.Bunnet (2007) General Geography in Diagrams

KISWAHILI

1. Kimbunga -H.Gora (Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili) (TUKI), 1994
2. Mapenzi Bora-S.Robert (Mkuki na Nyota)
3. Chungu Tamu-T.A MVUNGI (Tanzania Publishing house), 1985
4. Fungate ya Uhuru -M.S Khatibu (Macmillan and Aidan)
5. Vuta N'kuvute -Shafi (Mkuki na Nyota 1999)
6. Kufikirika-S.Robert (Mkuki na Nyota 2003)
7. Mfadhili –Hussein Tawa (Methew &stationery 2007)
8. Usiku Utakapokwisha-Mbunda Msokile 2007
9. Morani-E.Mbogo
10. Nguzo Mama-P.Muhando
11. Kivuli Kinaishi-
12. Kwenye Ukingo wa Thim-E.Hussein
13. Kunga za Fasihi na Lugha –M.Msokile (1992)
14. Fasihi-F.E.M.K.Senkolo 1984
15. Kitangulizi cha Tafsiri Nadharia na Mbinu-Mwansoko, H.J.M. (1996)
16. Nadharia ya Lugha Kidato chaTano na Sita Suluhaya, M.C. (2010) silabsi mpya.
17. Nadharia ya Fasihi (kipya) J.A Masebo Chapa ya Tisa.-Silabasi mpya.

MATHEMATICS

1. Basic Applied Mathematics by Respicius Kiiza (2010)
2. Mathematics for Class XI&XII by DASS, H.K&VERMA, R. (2000)
3. Pure Mathematics (Revised Edition) by M.F. Macrae(2011)
4. Pure Mathematics Volume I&2 by Backhouse, J.K (1985)
5. Core Mathematics for Advanced Level by L.Bostock
6. Advanced Level Mathematics by L.K.Shayo

7. Advanced Level Mathematics Vol I&II by Kinunda (1974)

ENGLISH
1. Macmillan Education Ltd 2000 Encounters from Africa, Macmillan
2. Ayi Kwei Amah, 1996, The Beautiful Ones are not Yet Born, EAEP
3. Chinua Achebe, 1991, A Man of the People, BAEP
4. Ndunguru 1999, Divine Providence, Mkuki na Nyota
5. Magala Nyago, 1985, The Rape of the Pearl Macmillan
6. Namige Kayondo, 1995 Vanishing Shadows, Macmillan
7. Danny Sato, 1983, His Excellency the Head of State, Macmillan
8. David Omowale, 2002, A Season of Welting, EAEP
9. Francis Lubuga, 1990, Betrayer in the City, Heinemann
10. Ngugi wa Thiong'o, et al 1982,I will Marry when I Want, EAEP
11. Bukenya, 1984, The Bride, EAEP
12. Okot Omitah 1991, Lwanda Magere Heinemann
13. Henrick Ibsen, 1974, An Enemy of the People, Eyre Matheuen
14. John Ruganda 2005, Black Mamba, EAEP
15. Charles Mloka, 2002, The Wonderful Surgeon and other Poems, Mkuki na Nyota
16. Tanzania Institute of Education, 1996, Selected Poems, Print pak (t)Limited.
17. The Real English Textbook for Advanced Level, Dr, Kadeghe Michael

PHYSICS
1. Advanced Level Physics $6^{TH}$ edition by Nelkon and Parker (1989)
2. Advanced Physics by Tom Duncan
3. Advanced Level Physics Paper 1&2 by E.Njau (2002)
4. Principles of Physics for Class XII&XI by S.Chand (2011)
5. A –level Physics Fourth Edition by Roger Muncaster (1993)

CHEMISTRY
1. Advanced Chemistry Physical and Industrial by P.Mathew (2006)
2. Essentials of Physical Chemistry by Arun Bahil,B.S Bahil &G.D Tuli (2012)
3. Organic Part A&B by A.Abdullah &M.H Nkunya
4. Inorganic Part A&B by J.S.Maro Guerman & M.Mikesewala (1989)
5. Physical Chemistry by Ddungu & J.B.A.Mihigo (1998)
6. Advanced level Inorganic Chemistry Part I&II by Tanzania Institute of Education (1995)
7. Organic Chemistry an Introduction by Jack E.Fernandez (1982)
8. Uderstanding Chemistry for A-Level Students
9. Conceptual Chemistry for Class XII&XI by S.K Jain (2011)
10. Advanced Level Chemistry, Fourth Edition by Ramsden (2000)

BIOLOGY
1. New Understanding Biology for A-level student by Glenn & S.Toole (1999)
2. Systematic and Classification by L.K Msaki (1993)
3. Biology, A Functional Approach by M.B.V Robert (1971)
4. Advanced Biology: Principle and Application by C.J.Clegg&D.G.Mackean (2000)
5. Biological Science by Taylor, et.al (1997)
6. S.Chand's Bioloy for Class XI&XII by P.S Verma &B.P.Pandey (2005)
7. Guide to Dissection by H.G.Q Rowett (2005)

.